JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO CHA UALIMU KOROGWE

Simu 027 2640540
027 2640847
Fax: 027 2640999
Email: korogwettc@gmail.com

Kumb. Na. KTC/Reg/Vol.1/123/06



S. L. P. 533
KOROGWE.

02/07/2020

Ndugu……

S.L.P. ……..

……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA UALIMU WA MASOMO YA SAYANSI NA HISABATI 2020/2021

1. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukujulisha kuwa **Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia** imekuchagua kujiunga na mafunzo ya **Stashahada ya Ualimu wa Masomo ya Sayansi na Hisabati)** katika chuo hiki kwa mwaka wa masomo **2020/2021**. Hongera sana.

2. TAREHE YA KURIPOTI CHUONI

Unatakiwa kuripoti chuoni tarehe **24.08.2020** ambapo baadae kutatolewa maelekezo (orientation) yahusuyo kozi yako na maisha ya chuoni. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **07.09.2020**.

3. MAHALI CHUO KILIPO

Chuo cha Ualimu Korogwe kipo katika wilaya ya Korogwe mkoa wa Tanga, kilometa mbili na nusu (Km 2.5) kutoka stendi mpya ya mabasi Korogwe mjini. Ukishuka kwenye basi tafuta bajaji zinazoelekea Hospitali ya Wilaya ya Korogwe (HOSPITALI YA MAGUNGA). Ukipenda unaweza kukodi Taxi au Bajaji ili ufike chuoni haraka. (kukodi usafiri wa bajaji nauli ni shilingi elfu moja hadi chuoni). Usitumie usafiri wa bodaboda ni hatari kwa usalama wako.

4. MAHITAJI MUHIMU

4.1 Maagizo ya Vyeti/Nyaraka

i. Vyeti vyote halisi vya kitaaluma (Academic Certificates) vya Baraza la Mitihani la Tanzania Kidato cha NNE (CSEE) na SITA (**Kwa wahitimu wa kidato cha sita**), vyeti vya kuhitimu Elimu ya Sekondari kidato cha NNE na SITA (Leaving Certificates)
ii. Vivuli vya vyeti (photocopy). Vyeti halisi vya taaluma vitabakia ofisi ya usajili kwa ajili ya uhakiki zaidi wa NECTA.
iii. Cheti cha kuzaliwa.
iv. Nguzo adili za chuo (sheria za chuo) iliyosainiwa na mwanafunzi na mzazi/ mlezi baada ya kukubaliana na taaratibu zote za chuo zilizoko katika fomu hii.

4.2 Ada ya Mafunzo

Ada ya mafunzo kwa mwaka ni Shilingi **450,000**/=. Ada hii inaweza kulipwa yote au kwa awamu mbili yaani kwa kila muhula. Malipo yafanyike kupitia mfumo wa malipo ya serikali kwa kutumia ***Control Number*** ambayo inapatikana Chuoni ofisi ya Mhasibu wa Chuo.

4.3 Michango Mingine

i. Ulinzi Tsh. **30,000/=** kwa mwaka.
ii. Ukarabati **25,000/=** kwa mwaka.
iii. Kitambulisho na Usajili Tsh. **20,000/=** kwa mwaka wa kwanza tu.
iv. Kukodisha Godoro Tsh. **10,000/=** kwa mwaka.
v. Vifaa vya Usafi na mazingira Tsh. **20,000/=** kwa mwaka.
vi. Huduma ya kwanza Tsh. **10,000/=** kwa mwaka.
vii. Michezo Tsh. **30,000/=** kwa mwaka.
viii. Serikali ya Wanachuo Tsh. **5,000/=** kwa mwaka.

Michango yote ambayo jumla yake ni Tsh. **150,000/=** zilipwe kwenye akaunti ya Chuo **NMB** yenye jina **PRINCIPAL KOROGWE T.C ACCOUNT No. 41501100012** na kuwasilisha *Pay in Slip* yenye jina la Mwanachuo.

Muhimu: Fedha ya matumizi binafsi au Fedha ya Ada isichanganywe na fedha ya michango.

4.4 Maagizo ya Vifaa vingine kwa wote

- Shuka mbili za rangi ya bluu bahari (Light blue).
- Koti jeupe la maabara (Lab coat) kwa watakaosoma masomo ya sayansi.
- Madaftari tisa (09) (**counter book quire 4**).
- Bunda moja la karatasi za fotokopi.
- Chandarua (neti) ya kuzuia mbu.
- Ndoo ya kutunzia maji ya matumizi yako chumbani.
- Picha: Lete picha mbili (2) passport size light blue background.
- Vifaa vya chakula; bakuli, sahani,kijiko na kikombe.

5. SARE YA CHUO:

Wanachuo wa Kike:

i. Sketi mbili nyeusi zisizo za kubana na ziwe ndefu kiasi cha kuvuka magoti (Kipimo cha urefu kiwe usawa wa goti na kisigino). Kila moja iwe na rinda boksi lenye muonekano wa V kuelekea chini) (**Tazama mchoro**)
ii. Mashati mawili ya mikono mirefu ya bluu bahari (light blue) na koti jeusi.
iii. Kwa wasichana wa kiislam watavaa suruali rangi nyeusi na nusu kanzu (Punjab) rangi ya bluu bahari (light blue) na Juba rangi ya bluu bahari lisilozidi vitanga vya mikono.
iv. Jozi mbili za viatu vyeusi vya kuchomeka vyenye visigino vifupi na jozi mbili za soksi nyeupe;
v. Tai ndogo ya rangi nyeusi (Butterfly tie)

Sare kwa Wanachuo wa Kiume:

i. Suruali mbili za rangi nyeusi zisizo za kubana wala kuchongwa. ***Suruali za jeans haziruhusiwi (*Tazama mchoro)**
ii. Mashati mawili ya mikono mirefu ya rangi ya bluu bahari (light blue) na koti jeusi la suit (kitambaa cha suruali na koti kisiwe na michilizi yeyote).
iii. Jozi mbili za viatu vyeusi vya kuchomeka na visivyo na visigino virefu na jozi mbili za soksi nyeusi;
iv. Tai ndefu ya rangi nyeusi.

Mavazi ya Michezo kwa wote

i. Tracksuit na bukta (light blue) na raba za michezo.
ii. T-shirt yenye nembo ya chuo inapatikana chuoni kwa gharama ya Tsh.**15,000/=** tu.

NB: **SARE HIZI ZITAKAGULIWA KABLA YA KUSAJILIWA**.

6. MAAGIZO KUHUSU AFYA

Unatakiwa kuzingatia yafuatayo kwa ajili ya ustawi wa afya yako kwa kipindi chote cha mafunzo:

- Uje na fomu ya afya (iliyoambatanishwa) ikiwa imejazwa kikamilifu na Mganga wa hospitali inayotambuliwa na serikali, ili kuthibitisha hali ya afya yako.
- **NI LAZIMA** kuja na **kadi ya Bima ya Afya kwa ajili ya matibabu yako yote**.
  Chuo kinatoa huduma ya kwanza tu. Kama huna unashauriwa kutembelea ofisi za Bima ya Afya (NHIF) ili kujiunga.
- Chuo hakitoi chakula maalum (Special diet)

7. MAWASILIANO

Mahitaji na maagizo yote yatakaguliwa wakati wa usajili. Kwa maelekezo zaidi unaweza kuwasiliana na Msajili wa Chuo kwa namba: **0719 813099, 0784 617514**, **0621 013713; 0787 420702; na kwa mahitaji ya Control number 0715 668838.**

8. MWISHO

Jumuiya ya Chuo inatarajia kwamba utaonyesha tabia na mwenendo mwema na kuzingatia maelekezo ya walezi wako katika muda wote wa mafunzo yako kwani *Ualimu Bora huanzia Chuoni*. Kauli mbiu ya Chuo chetu ni: **Mwalimu kwa Mfano.**

Karibu sana Chuo cha Ualimu Korogwe

Hassan A. Ismail
MKUU WA CHUO

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A

Principal,
Korogwe Teachers' College,
P.O. Box 533
KOROGWE

To the Medical Officer,

.....

.....

.....

RE: Mr/ Mrs/ Miss .....

Please examine the above named to his/ her physical and mental fitness for a full time teacher education course. The examination should include the following categories (I - IV), each category or subcategory of which will render the applicant ineligible in case of defect. Pregnancy (category iv) will also render a girl candidate ineligible for the course, including category V.

I. (a) Eyesight (b) Hearing (c) Speech (d) Limbs (e) Venereal disease (f) Leprosy

(g) Epilepsy (h) Epilepsy (i) Tuberculosis

II. Neuroses

III. Other serious diseases

IV. Pregnancy

V. Mental and Physical Fitness

NB: the applicant will not be admitted unless this is duly filled.

Date .....

Signature .....

PART B **MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/ she is physically fit / unfit and mentally fit / unfit to a fulltime teacher training course.

I . a) Eyesight .....

b) Hearing .....

c) Speech .....

d) Limb .....

e) Venereal Diseases .....

f) Leprosy .....

g) Epilepsy .....

h) Typhoid .....

II. Neuroses

III. Other serious diseases

IV. Pregnancy

Date ..... **Signature** .....

Station ..... **Designation** .....

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO CHA UALIMU KOROGWE
NGUZO ADILI ZA CHUO

1. Kibali cha kulala nje ya chuo,kutoka nje ya mipaka ya chuo au kwenda nyumbani kwa mfanyakazi hutolewa na mkuu wa chuo au ofisi ya uadili kwa niaba.

2. Kila mwanachuo sharti awahi,darasani,mstarini,bwaloni/ukumbini,katika kazi za nje mara aitwapo kwa kengele.Ni marufuku mwanachuo kulala bwenini bila kibali cha mkufunzi wa zamu au mganga wa chuo.

3. Mwanachuo hatajishirikisha katika siasa wakati wote wa mafunzo hapa chuoni,anatakiwa kila wakati kutumia busara katika kufanya maamuzi yake,kutimiza wajibu kama utakavyoelekezwa na uongozi pamoja na wafanyakazi wengine wa chuo na uongozi wa serikali ya wanachuo,na kufuata kanuni na taratibu zote za serikali ya jamhuri ya muungano wa Tanzania.

4. Mwanachuo hatakashifu,kuzomea,au kuguna wakati viongozi wote wa ndani na nje ya chuo wanapozungumza bali atauliza swali ili aelezwe zaidi. Jizuie kufanya jambo lololote litakaloleta tafsiri ya dharau kwa yeyote.

5. Mwanachuo haruhusiwi kupika chakula bwenini au kuwa na vifaa vyovyote vinavyoweza kuleta hatari ya moto kama mafuta ya taa, petrol, mishumaa, heter, au pressure cookers.

6. Mwanachuo hataruhusuwi kuwapeleka wageni mabwenini au kumkaribisha bila uongozi wa chuo kuwa na taarifa.

7. Kila mwanachuo anatazamiwa kujipenda,kuwa na maarifa na moyo wa kujituma,kutunza mali za serikali,mali za chuo na watu wengine.

8. Mwanachuo lazima avae mavazi ya heshima na safi wakati wote,kutunza nywele vizuri,kutonyoa kipara,kufuga ndevu na sharafa,kuacha kucha ndefu na kuvaa mapambo yasiyoruhusiwa.

9. Ni marufuku mwanachuo kumpotezea mwanachuo mwenzake muda katika mambo yasiyo ya msingi hasa mikutano isiyo rasmi,vikao vya gizani na kuitisha vikao visivyo na kibali kutoka ofisi ya uadili.

10. Mwanacho haruhusiwi kutumia ulevi wa pombe,bangi na madawa ya kulevya au sigara kwa kipindi cha mafunzo yake.

11. Tabia za uasherati,ushoga na ubakaji ndani na nje ya chuo itakunyima nafasi ya kuendelea na mafunzo ya ualimu.

12. Mwanachuo haruhusiwi kuanzisha ugomvi,kumpiga mtu au kupigana wakati wote wa mafuzo ya ualimu.

13. Kupatikana na kosa au kesi ya **Wizi** na makosa ya jinai ukiwa mafunzoni utakuwa umejifukuzisha chuo na mafunzo ya Ualimu.

FOMU YA KUKUBALI NAFASI NA NGUZO ADILI ZA CHUO

I. **MWANACHUO**

Jina la Mwanachuo……

Anuani……

Mimi……

nimekubali kujiunga na Chuo cha Ualimu Korogwe. Nimesoma maagizo ya Chuo kwa makini na kuyaelewa. Naahidi kuwa mtiifu na nitazingatia sheria, na taratibu zote za Chuo kama nitakavyoelezwa.

Saini ya Mwanachuo…… Tarehe……

II. **MZAZI/MLEZI**

Mimi……..

Mzazi/Mlezi wa…… ……..

Nimesoma kwa makini maagizo ya chuo yaliyotolewa kwa mtoto wangu. Nimekubali

mwanangu achukue nafasi hiyo. Naahidi kuwa nitashirikiana na Uongozi wa chuo katika kumkuza na kumlea mwanachuo huyu kielimu na Kitabia kuwa mwalimu wa mfano katika jamii.

Saini ya Mzazi/Mlezi……Tarehe…….

ZINGATIA/SISITIZO

- Mzazi/Mlezi hakikisha mwanao amezisoma Sheria zote za chuo zilizoambatanishwa

  na mzitafakari ndipo usaini fomu hii.

KIAMBATANISHO NAMBA MOJA (1)
NB: SARE ZISIWE NGUO ZA MITUMBA.

(a) Suruali



PICHA NA.1

(b) Sketi



PICHA NA.2

MUHIMU:

1. Mavazi yako kwa wakati wowote mwingine ni **LAZIMA** yaakisi maadili bora ya Ualimu. Nguo za kubana, pensi, vimini/vitop au zenye mipasuo mikubwa haziruhusiwi hapa chuoni.